


Pambazuko

Toleo Namba 060

Jumatatu Februari 5-11 2024



Jicho la Tai CCM ya Makonda vs Serikali ya Samia **Uk. 5**



Waasi M23 DR Congo wahaha

● *Ni baada ya
JWTZ kuingia*

Uk. 6

**Ujerumani
yaliasa
Pambazuko,
yapongeza**

Uk. 8



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Sasa tumefika 500,000+. Aksanteni

AWALI ya yote tunapenda kuwatakiwa wasomaji wetu wote heri na neema tele kwa kila mmoja wakati “anapambana” kuhakikisha maendeleo binafsi ya yale ya taifa, yanapatikana.

Tunaamini kwamba mazonge na madhila yanayoikumba dunia na hasa nchi na kusababisha madhara makubwa, hayatatokea tena – labda yale yaliyo juu ya uwezo wa binadamu.

Hata hivyo, bila kujali yepi yamo ndani ya uwezo wa binadamu, basi kila mabaya yaliyotokea mwaka jana yawe funzo kubwa kukabili na kuepusha hasara ya mali na nguvu kazi kwa mwaka huu.

Pambazuko likiwa linawafikia wasomaji wake karibu miezi 20 sasa tangu kuanzishwa kwake, tunapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza sana wasomaji wetu, wachangiaji wa makala, safu na vibonzo, na wapenzi wote wa Pambazuko kwa ujumla wake wanaoendelea kutusoma, kusambaza na kutupatia ushauri wa kuboresha gazeti hili la umma.

Wakati tukianza gazeti hili, linalotolewa bila malipo kila wiki, wengi walidhani ni ndoto, maswali yakawa mengi; mengine ya kukatisha tamaa, lakini kwa kuwa tulikuwa na nia, lengo limetimia na tunaendelea kuimarika na kusonga.

Katika kipindi hiki, habari nyingi zimeandikwa kwa weledi mkubwa, picha nyingi zimetumika, katuni na vibonzo vimesheheni, makala zenye kuelimisha na kukanya yameandikwa na zaidi sana safu zetu zimeendelea kuwa bora zaidi.

Tunawashukuru sana watu wote wanaoendelea kututia moyo kwamba, pamoja na kusambaza gazeti bure,

ubora wa yale yanayochapwa na Pambazuko hauna shaka hata kidogo, ndiyo maana gazeti linaendelea kupendwa na kusambazwa zaidi na zaidi.

Katika kipindi hicho chote, habari na makala nyingi zimechapwa na Pambazuko na matokeo ya habari hizo yanaweza kupimika – kwa maana ya kusukuma hatua kuchukuliwa.

Moja ya habari kubwa ambayo matokeo yake yamepatikana haraka na yanapimika ni habari kubwa iliyoandikwa Desemba, 2022 iliyokuwa ikielezea namna Wizara ya Afya inavyokwamisha ustawi wa afya kwa Watanzania kwa kushindwa kutoa leseni kwa hospitali binafsi, licha ya kukamilisha taratibu zote na baada ya kukaguliwa na wizara hiyohiyo.

Baada ya habari ile wiki iliyofuata, wizara ilianza kutoa leseni na bado inaendelea kutoa kwa hospitali binafsi zilizokidhi viwango.

Pamoja na matokeo hayo, na wakati tukiwa ndiyo tunaendelea kusonga na mwaka huu mpya wa 2024, tunahimiza serikali, taasisi, jumuiia, ofisi zote na zile za binafsi kufanya kazi kwa bidii kwa kuwatumikia vyema Watanzania ili kuwa chachu ya kukuza uchumi wa familia na taifa.

Pambazuko tunasema tena, aksanteni sana kwa kuwa pamoja nasi kwa miezi 20 hata kutufanya kuwa chombo kinachosambazwa na kusomwa zaidi Tanzania.

Sasa familia ya Pambazuko inawafikia watu zaidi ya 500,000 kila wiki bila kukosa.

Endeleeni kutuunga mkono ili tuboreshe zaidi kazi zetu za kulitumikia taifa.

TANZANIA SASA KUMENOGA...



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba akiitangaza Tanzania na sababu za wawekezaji kuweka mitaji yao huko, mbele ya wafanyabiashara wakubwa, viongozi wa siasa na jamii ya Waitaliano katika Jiji la Rome, Jumanne iliyopita. (Picha na mtandao wa X).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Ungwana ni kusaidiana katika shida zaidi, kwenye raha - mengi mabaya hujificha. Hivyo, ukitaka kutambua watu wako wa karibu na namna wanavyokupenda, basi watazame wanavyojitoa kwako wakati wa shida na utabaini nani ni nani - Msemo wa Kilatini.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023**

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandaa: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscana

Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

igmpesa | Tigo | Airtel | M-Pesa | Airtel | hola | 0744

CCM ya Makonda vs Serikali ya Samia

Na Igo AI

TAI usiku wa kuamkia leo hajalala kabisa. Amesikika akigongagonga ukuta, huku akitamka maneno yaliyoshindwa kusikika vyema.

Sauti aliyokuwa akiitoa ni kama vile “ananena kwa lugha,” maana siyo mwandishi wake wala kijana wa kazi walioambulia maana ya kile alizungumza.

Lakini kwa kuwa wawili hao; mwandishi na kijana wake wa kazi wanamwelewa vyema, hawakushughulika naye sana usiku huo, maana amejitokea utaratibu wa kutogongewa chumbani mara anapoingia kujipumzisha.

Alhamdulillah! Kumekucha na Tai akawahi mezani kwa ajili ya kustaftahi. Mezani akakuta ameandaliwa chai yake ya sturungi, mayai mawili ya kukaangwa na viazi vitamu vilivyochemshwa.

Wakati anaendelea kupata kifungua kinywa, akasikika akilalama kwamba ni bora asingekuwa msomi, mfuatiliaji wa mambo na zaidi sana anafikiria kuacha kusoma magazeti, kusikiliza redio wala kutazama runinga.

Kisa ni nini? Anadai anapata msongo wa mawazo kila uchao; kwamba hajui nani ni nani katika chama chake cha CCM na anavurugwa zaidi kuona serikali eti “hajitambui.”

Tai anadai kumuona Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (Itikadi,Uenezi na Mafunzo) wa chama chake, Paulo Makonda akiwa anazunguka huku na kule akisikiliza na “kutatua” kero na shida za watu, kazi ambayo ilipaswa kufanywa na watendaji wa serikali hata kabla chama hicho tawala hakijatia mguu.

Tai anashangaa kusikia kuwa kuna wasaidizi wa Rais Samia Suluhu Hassan kila mahali, lakini kumbe ni kama hawafanyi kazi. Hawawezi kutatua shida za wananchi.

“Hivi hawa wasaidizi wa Rais Samia wanafanya kazi gani huko walikopangiwa kazi, mbona kama wamelala na kulewa tu. Mbona wanakula mishahara ya bure



Paulo Makonda, Katibu Uenezi wa CCM

tu! Akang’aka.

Tai akanyanyuka kutoka kwenye meza, akapiga kelele; “ningekuwa Rais Samia ningefukuza wote na kuweka wengine, inaonekana hakuna anayefanya kazi; kila anakopita Makonda ni shida tu; hawa wakuu wa wilaya, mikoa na wengine wamewekwa kwa sababu gani, au ni kugawana mishahara tu?”

Tai akamuita mwandishi wake na kumtaka aandike swali na kuliweka gazetini kwamba ni nani hasa anayesababisha kero na shida kwa wananchi; ni chama ama serikali na nani anatakiwa kuzitatuwa?

Akasema inavyoonekana walioyasababisha matatizo hayo wanayakimbia na kuacha mzigo kwa chama, sasa kwanini wasifukuzwe.

Tai akasema mfumo wa serikali kusimamia kazi na kutatua madhila ya wananchi ni kama haufanyi kazi. Kwamba serikali imelala na hakuna wa kuiamsha kwenye usingizi mzito, ndiyo maana Makonda anakuja na utaratibu wa mahakama kama za kangaroo – kwa kufoka na kukemea huyo na yule na kuwaonesha wameshindwa kazi.

Sasa ni vita ya Makonda na CCM yake dhidi ya watendaji wa serikali ya Rais Samia, ambayo Tai anadai haitaisha.

Habari

Waasi M23 DR Congo wahaha

Na Mwandishi WETU

SASA ni dhahiri kwamba wapiganaji wa vikosi vya waasi wa M23 walioko mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wana “matumbo joto” baada ya majeshi ya Tanzania kuwasili huko.

Taarifa za ndani ya M23 na washirika wao, zilizofikia Pambazuko juzi – Jumamosi na jana, Jumapili, zinaeleza kuwa vikosi hivyo vya waasi, vimeanza kujipanga upya kukabili nguvu kubwa ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ambayo imeongezwa kwenye vikosi vya kulinda amani DRC vya Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Nguvu ya mashambulizi, weledi, vifaa na ujuzi wa kukabili adui, hasa katika viunga vya medani, ni mhimili wa wapiganaji wa JWTZ, hivyo kuwatisha waasi hao ambao wamekuwa wakisumbua amani na maendeleo ya DRC.

Pambazuko limeelezwa kuwa kuwasili kwa wanajeshi wa JWTZ huko mashariki ya DRC, kumewatia “jambajamba” waasi hao wa M23 na sasa wameamua kuvunja moja ya kambi zao kubwa ili kurudi nyuma kujipanga kwa kuogopa majeshi ya Tanzania.

Hata hivyo, katika kuonesha umma wa DRC na dunia kwamba waasi hao wako imara, jana walitoa taarifa kupitia mitandao ya kijamii kwamba wako tayari kukabili “nguvu ya Watanzania” ndani ya majeshi ya SADC.

Katika taarifa yao, M23 walidai kuwa watajibu mashambulizi na kwamba wamejipanga kwa umadhubuti mkubwa kujibu mashambulizi makali ya silaha za vikosi vya JWTZ vilivyotumwa mashariki mwa Congo.

Msemaji wa waasi wa M23, Lawrence Kanyuka alijitapa kwamba wao hawaogopi Watanzania na majeshi yao, hata kama wako imara, lakini watambue kwamba watakumbana na “chuma kilichowashinda wengi.”

Kanyuka alijitapa kwamba



Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hasan

wataangamiza wanajeshi wengi waliotumwa “kuwamaliza wao” hata kama wana nguvu kubwa kiasi gani katika vita.

Alidai kwamba M23 wanatambua kuwa majeshi ya SADC yameongeza nguvu ili kwenda kuuwa wanajeshi wake, lakini nao hawatakuwa wanyonge na kwamba watatumia uzoefu wao kuwakamata wanajeshi hao na “kuwafunza adabu.”

Pambazuko linazo taarifa kwamba wapiganaji wa JWTZ wamepangwa kuwepo katika eneo la Masisi, ambako waasi hao wa M23 wamekuwa wakiweka kambi na ngome yao kubwa ili kufanya mashambulizi dhidi ya wananchi wasiokuwa na hatia wa DRC.

Inaelezwa kuwa katika eneo hilo la Masisi na jirani zao, waasi wa M23 wamekuwa “wakorofi mno” kiasi cha kuyapiga na kurejesha nyuma majeshi ya DRC, hatua ambayo imewafanya waasi hao kutamba kwamba eneo hilo ni mali yao.

Hata hivyo, kuwasili kwa JWTZ kumewakimbiza na sasa waasi hao wanaelezwa kusogea ndani ya msitu ambako inadaiwa “wanakwenda kujipanga” ili warudi na nguvu mpya ya kuwakabili JWTZ.

Eneo la Masisi limeshuhudia mapigano makali kati ya wanajeshi wa Congo na waasi wa M23 katika miezi ya hivi karibuni, ambapo idadi kubwa ya watu wamepoteza maisha.

Shamte: kuna mvutano Ikulu Zanzibar

Na Marzuk ALI, Zanzibar

MAONI ya kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Baraka Mohammed Shamte baada ya kujiuzulu Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohammed Said, yanachimbua taswira ya kuwepo mvutano wa kiutendaji kwenye uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kada huyo ameliambia Pambazuko jana mjini Zanzibar kwamba dalili zinaonesha kuwepo kwa mvutano wa kiuongozi na kwamba “huenda mambo hayaendi sawa,” ndani ya Ikulu ya Rais Mwinyi.

Shamte amebainisha kwamba amepata taarifa kwamba walikuwepo baadhi ya mawaziri waliopanga “kuachia ngazi,” kabla ya Simai, lakini woga na kuendelea kuvuta subra kuliwaponza hadi rais akatangaza mabadiliko ya baraza lake la mawaziri.

Amesema kuwepo tu kwa fununu kutoka Ikulu kwamba wapo wateule wa rais wanapanga kijiuzulu, ni ishara ya “mambo kutokuwa sawa.”

Simai alijiuzulu Januari 26 mwaka huu kwa alichosema anakabiliwa na “mazingira yasiyo rafiki” katika kutekeleza majukumu aliyopewa ya kumsaidia Rais Mwinyi, na kwamba anaona hatakuwa anamsaidia kiongozi huyo wa nchi ikiwa akiendelea kuwepo na dhamana aliyompa.

Wakati huohuo, wadadisi wa masuala ya uongozi, wanasema CCM inapaswa kuwa makini kudhibiti mvutano ya ndani kabla haijavuruga mazingira mazuri ya kujengea Zanzibar uchumi mkubwa na kukihakikishia chama ushindi utakapofika uchaguzi Oktoba 2025.

Siku moja tu baada ya Simai kujiuzulu, Shamte alisikika akisema kupitia taarifa ya mitandaoni kuwa kujiuzulu kwa Simai kumemshtua kwani anavyomjua ni mtu wa “karibu sana” na Rais Mwinyi, kuna jengeka hofu ya kuwepo jambo



Rais Dkt. Mwinyi

kubwa ambalo haliko sawa katika uongozi wa Dkt. Mwinyi.

Anasema Simai hakueleza undani kwa kuamini anatii kiapo cha uwaziri aliyopewa, lakini lilikuwa jukumu la Ikulu kutangaza sababu.

Anasema; “lazima kuna kitu na kwamba tukijidai kukifichaficha, tukijidai kujifichaficha, haitakuwa waziri mmoja kufanya hivi. Haitakuwa kabisa, naamini wako wanaoamini kufanya vile, basi tu wanahofu na wasiwasi, mwenzako keshakutoa hofu kwa sababu ni sehemu ya demokrasia.”

“Ni jambo lina maana kubwa, na mimi nina imani si muda mrefu watajitokeza wengine. Kwa sababu gani, hofu imetoka. Kitu kinachoumiza watu sasa hivi ni vitisho,” anasema na kungeza “au kupikiwa majungu kuonekana unampinga mkubwa, ninampinga vipi? Napinga jambo la serikali nami ni sehemu ya serikali. Naona jambo silo, yako mambo yanamkifu mtu anakaa ofisini hana uhuru kama ofisi si yake Waziri, kafika mahali kaona bora kujiuzulu, Alhamdulillah,” anaongeza kada huyo.

Shamte aliyejitokeza wazi kusema hakumuunga mkono Dkt. Mwinyi wakati wa kugombea urais wa Zanzibar mwaka 2020, anajulikana alivyo mstari wa mbele kumkosoa aonapo tatizo, na endapo kuna jambo analoamini haliko sawa na linakidhoofisha chama chake, basi hulisema hadharani ili lirekebishwe.

Habari

Ujerumani yaliasa Pambazuko, yapongeza

Na Mwandishi WETU

GAZETI la Pambazuko limehimizwa kuibua changamoto za wananchi, kuonya watendaji wabovu na wasiwajibika, ili kuwa chombo cha kuwasemea wananchi.

Ushauri huo umetolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, na Naibu Balozi wa Ujerumani Tanzania, Dkt. Kathrin Steinbrenner, wakati akizungumza na Simon Mkina, Mhariri Mkuu wa Gazeti la Pambazuko.

Mazungumzo yao yalijikita katika mazingira ya sasa ya kupashana habari Tanzania na namna uhuru wa maandishi wa habari unavyoatamiwa na serikali.

Balozi Kathrin alisema pamoja na kutojua vyema Kiswahili, lugha ya gazeti hilo la kila wiki, lakini amekuwa akifuatilia habari zake na kwamba limeonekana kujipambanua na kujiondoa kwenye “habari za kawaida za kila siku.”

Amesema Tanzania inatakiwa kuwa na vyombo vya habari ambavyo vinawasemea wananchi wa kawaida na siyo kuwa vipaza sauti vya “wakubwa na watu wenye uwezo.”

Balozi Dkt. Kathrin akasema ni vyema sasa Pambazuko lisimame na kuwa chanzo cha mwanga wenye matumanini kwa Watanania ambao, kwa kiasi kikubwa wanakosa habari zenye kusaidia maendeleo yao.

“Unapokuwa na chombo cha habari, na kazi yake ikiwa kuandika wakubwa wanafanya nini na kuaweka pembeni wananchi wa kawaida, tena wapigakura,

basi chombo hicho kinakosa maana ya kuwepo, nyie badilikeneni,” ameongeza balozi huyo.

Amesema vyombo vya habari vya Tanzania, kama ambavyo vile vya Ujerumani vinafanya kazi, vinapaswa kuibua rushwa, watendaji wabovu wa serikali, wezi wa mali ya umma na zaidi sana, vigeuke kuwa vipaza sauti vya wananchi wanaokosa sehemu ya kukimbilia kueleza changamoto zao.

“Nye Pambazuko mjaze nafasi hiyo kwa sasa, bado mna wajibu wa kuibua mambo yanayopaswa kuwafikia wenye kutoa uamuzi ili hatua thabiti zichukuliwe,” akaongeza.

Mkina, ambaye pia ni Rais wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) aliahidi kuendelea kulisimamia Pambazuko na kuwa “chombo cha wananchi kwelikweli,” ili kuchochea mabadiliko yenye tija kwa Watanania.

Akasema tangu kuanzishwa kwa Pambazuko, pamoja na uchanga wake, limeweza kuchochea mabadiliko kadhaa ambayo yanaweza kuthibitishwa na waanchi wenyewe.

Alimjulisha balozi huyo kuwa hadi sasa Pambazuko linasambazwa kwa njia ya WhatsApp na kwamba lina wasomaji waliosajiliwa zaidi ya 10,000 huku wafuatiliaji wake wakikadiriwa kufikia 500, 000 kila linapotoka.

Gazeti la Pambazuko linalosambazwa kila Jumatafu, huwafikia wasomaji wake bila malipo na kwamba linaendelea kuboresha maudhui na ukijikita katika habari za chunguzi na uchambuzi.



Simon Mkina akizungumza na Naibu Balozi wa Ujerumani Tanzania, Dkt. Kathrin Steinbrenner. Katikati ni Mkurugenzi Mkazi wa Tanzania wa Taasisi ya KAS, Dkt. Tilmann Feltes (Picha na Hendrik Sittig)



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Serikali itumbue jipu la matapeli tiba asili

Na Rashid MTAGALUKA

HAKUNA shaka kwamba shinikizo la juu la damu (BP) na kisukari, ni miongoni mwa magonjwa maarufu nchini yasiyoambukiza, yenye dawa ya kuyatuliza tu.

Kwa kuwa magonjwa haya huchangia kwenye matatizo ya kiharusi (stroke) pamoja na tatizo la figo kwa zaidi ya asilimia 25 ya wagonjwa wote, baadhi ya madaktari wameyaita kwa utani kuwa ni "mtu na binamu yake!"

Ingawa historia inaonesha kuwa magonjwa haya yamegundulika tangu mwaka 1920, lakini mpaka sasa madaktari bingwa wote pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO), wamekubaliana dawa ya kutibu hasa haijapatikana.

Hata hivyo, ni jambo la kawaida siku hizi kumsikia tabibu wa tiba asili kupitia kwenye vyombo vya habari, ama akitangazwa au akijitangaza kuwa ni bingwa wa kutibu magonjwa haya.

Kinachoshangaza zaidi ni kuona watu hao wanafanya 'maigizo' haya mbele ya macho ya viongozi waliopewa dhamana ya kulinda afya za Watanzania kwa mujibu wa katiba na ambao wanajua kuwa kisayansi ni ngumu kwa mgonjwa wa kisukari kupona, hata kwa kutumia mitishamba!

Kusema hivi hakumaanishi nimegoma kutambua uwezo mkubwa walionao baadhi ya matabibu wetu katika kutumia miti na matunda kutibu magonjwa mbalimbali, la hasha!

Kama ni matumizi ya tiba asili, wenzetu India inaelezwa kuwa ni mabingwa kwelikweli katika kutumia mitishamba barani Asia, lakini kwa mujibu wa machapisho yaliyotolewa na mamlaka ya madaktari nchini India, kuna watu milioni 75 wanaugua kisukari, huku watu milioni 65 wakibanwa na shinikizo la juu la damu.

Na watazama tu kama wanasayansi nchini



Waziri wa Afya - Ummu Mwalimu

India pamoja na madaktari wao bingwa wa tiba asili na mbadala wamezidiwa na hawa wa kwetu kitaaluma, au sisi hapa matabibu wetu wanatumia teknolojia na miujiza gani 'kuwaponesha' wagonjwa wa kisukari na BP?

Je, wewe msomaji wangu, umewahi kuoneshwa mgonjwa walau mmoja tu aliyehibitishwa kisayansi kuwa na kisukari na shinikizo la juu la damu, kisha akatibiwa na matabibu wetu hao wa kiasili na akapona?

Kwa mujibu wa Profesa Khamis Malebo, Mwenyekiti wa Baraza la Tiba Asili Tanzania, kisayansi hakuna tiba ya magonjwa haya, bali kuna dawa za kusaidia kupunguza kiwango cha sukari mwilini.

Kama aliyosema Profesa Malebo ni ya kweli, hili jipu la watu kujitangaza wanatibu ugonjwa huu kwa lengo la kujipatia fedha, linaachwa mpaka lini?

Bila mamlaka zilizopewa meno kisheria kuchukua hatua, tutegemeo huko mbele vifo vingi vya watu wanaokula mizizi kutibu kisukari, badala ya kufuata ushauri wa madaktari wa kutumia dawa zilizohibitishwa na wataalamu kwa ajili ya kuchochea uzalishaji wa insulin mwilini.

•Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546 na barua pepe:mtagaluka@gmail.com

Habari

Watoto wenye uzito mkubwa wachunguzwa

Na Tryruckia MFINANGA

WATOTO wawili wa familia moja - wakazi wa Makole, Dodoma, wenye uzito mkubwa uliopitiliza, wamefikishwa Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila kwa ajili ya uchunguzi na tiba.

Kitabibu, watoto hao wenye miaka saba na mwingine mitano, walifikishwa jana hospitalini hapo tayari kuanza taratibu za kugundua changamoto za afya zinazowasibu hata kuwa na uzito mkubwa unaoongezeka kila uchao.

Daktari bingwa wa magonjwa ya dharura, Dkt. Asha Iyulla amesema wamewapokea watoto hao na kuanza kuwafanyia vipimo vya awali ikiwemo kuwapima uzito ambapo wamebaini mkubwa ana uzito wa kilo 76 na mdogo ana uzito kilo 62.

“Vipimo hivi tulivyofanya leo (jana) ni vya awali, kesho (leo) watafanyiwa vipimo vya ziada ikiwemo kupimwa wingi wa mafuta kwenye damu katika kliniki yetu ya uchunguzi na matibabu ya wingi wa mafuta kwenye damu pamoja na kufanya vipimo vingine ili kubaini tatizo



Dkt. Asha Iyulla

linalowakabili” ameegeza Dkt. Asha.

Mama mzazi wa watoto hao, Vumilia Elisha amesema amefurahishwa na mapokezi aliyoyapata katika Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila kwani yamempa faraja na matumaini ya watoto wake kupona maradhi.

Kuletwa kwa watoto hao kunafuatia kauli ya mkurugenzi mtendaji wa hospitali hiyo, Prof. Mohamed Janabi kuwa hospitali ipo tayari kutoa huduma za uchunguzi na matibabu kwa watoto hao ambao mama yao alionekana

akiomba msaada kupitia video na picha iliyokuwa ikisambaa kwenye mitandao ya kijamii.

Gazeti la Pambazuko linafuatilia maendeleo ya afya za watoto hao na litakuwa likuutaarifu umma maendeleo yao, huku uongozi wa gazeti ukiwataki heri kwa uchunguzi na matibabu ya watoto hao.



Mtoto mmoja akiandaliwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa awali. Picha zote na Hospitali ya Muhimbili

Tanzia: Lala salama Rais Hage Geingob

Rais wa Namibia Hage Geingob Ramefariki dunia usiku wa kuamkia leo.

Kifo cha kiongozi huyo kimetokea wakati akiendelea kupatiwa matibabu kwenye moja ya hospitali maarufu zilizopo kwenye mji mkuu wa nchi hiyo, Windhoek. Serikali ya nchi hiyo haikutaka kutaja jina la hospitali alokolazwa kwa matibabu.

Makamu wa Rais wa Namibia, Nangolo Mbumba alitangaza jana kuwa Rais Geingob alifariki dunia mapema asubuhi ya leo Jumapili, Februari 4, 2024. Habari zinaeleza kuwa alipoteza maisha saa 8:12 usiku.

Mbumba ameeleza kuwa wakati wa kifo chake, pembeni mwa kitanda alicholazwa kiongozi huyo, alikuwepo mke wake, Monica Geingos na watoto wake.

Kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 82 alikuwa akiugua saratani na yeye mwenyewe aliueleza umma juu ya tatizo hilo mwezi uliopita.

Ofisi yake ilitangaza kuwa kiongozi huyo wa Namibia alitarajiwa kusafirishwa kwenda Marekani kwa matibabu zaidi na angerejea Namibia Februari 2, 2024.

Rais Geingob aliingia madarakani kwa muhula wake wa pili na wa mwisho mwaka 2015.

Taarifa zinaeleza kuwa Rais Geingob alifanyiwa upasuaji mwaka jana, ambapo mwaka 2014 aliwahi kutangaza kwa umma kuwa alikuwa amepona saratani ya kibofu.

Namibia inatarajia kuingia kwenye uchaguzi wa rais na wabunge mwezi



Novemba mwaka huu. Rais Geingob hakuwa mgombea kwani katiba ya nchi hiyo inamkataza.

Chama tawala cha Swapo, ambacho kimekuwa madarakani tangu uhuru mwaka 1990, kilikuwa kimekamilisha mchakato wa kumchagua mgombea wake, ambapo mwanamama, Nandi-Ndaitwah alipitishwa kuwa mgombea urais.

Nandi ambaye kwa sasa ni naibu waziri mkuu, endapo atachaguliwa kuwa kiongozi wan chi hiyo, basi atakuwa rais wa kwanza mwanamke wa nchi hiyo.

Pambazuko tunawapa pole Wanamibia wote na hasa familia yake kwa msiba huu.

Lala salama Hage Geingob.

Wazo Binafsi

Tumeletewa tume huru isiyokuwa huru

Na Mwandishi WETU

NI muda mrefu sasa Tanzania imekuwa kwenye shinikizo la kutaka kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi kwa lengo la kuwa na chombo ambacho kuitaleta usawa katika kila uchaguzi, hasa wa nafasi za kisiasa.

Baada ya madai hayo ya muda mrefu, wiki iliyopita Bunge limeamua kuja na jibu lake – kubadilisha jina kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi na sasa iitwe Tume Huru ya Uchaguzi.

Hili ni jibu jepesi sana kwa sababu uhuru wa tume ya uchaguzi haupo kwenye jina. Uhuru wa tume yoyote ya uchaguzi ipo katika misingi fulani ambayo ndiyo inaongoza na kusimamia utendaji wa tume husika.

Tume yoyote ya uchaguzi ikiwa na misingi hiyo mizuri, basi hata neno huru lisipokuwa sehemu ya jina lake, basi hiyo itakuwa Tume Huru.

Lakini, kwa upande mwingine, tume ikiitwa Tume Huru ya Uchaguzi wakati uendeshaji wake hauzingatii ile misingi ya tume huru, basi tume hiyo haitakuwa huru pamoja na kuwa jila lake lina neno huru ndani yake.

Kuna misingi kama mitano muhimu ambayo inaifanya tume yoyote ya uchaguzi kuwa huru; msingi wa kwanza ni uhuru wa tume kufanya kazi yake; mwa pili ni tume kutopendelewa katika utekelezaji wa majukumu yake; msingi wa tatu ni uwazi; msingi wa nne ni kufanya kazi kwa weledi na msingi wa tano, ni tume kutokuwa tegemezi katika masuala ya kifedha.

Ikumbukwe kuwa misingi hii siyo tu kuwa inatakiwa iwe kwenye sheria inayounda tume, bali ionekane kutendeka wakati tume ikiwa inafanya kazi zake.

Kinyume cha hapo litabakia suala lilelile la kuwa na jibu jepesi kwenye swali gumu.

Katika mabadiliko ya sheria yaliyopitishwa na Bunge wiki iliyopita, mtu atakeyeongoza hiyo itakayoitwa



Spika wa Bunge Tulia Ackson

Tume Huru ya Uchaguzi ataendelea kuwa mtumishi wa umma.

Zimetolewa sababu kadhaa za kihalalisha hilo, lakini ikumbukwe kuwa Mahakama Kuu ilishawahi kutoa hukumu kuwa kuwatumia wakurugenzi wa halmashauri, ambao ni watumishi wa umma, kusimamia uchaguzi, siyo suala mujarabu iwapo tunataka kuona tume ikifanya kazi kwa uhuru.

Moja ya kasoro kubwa zinazoifanya tume ijayo isiwe huru hata kama jina lake linasema hivyo, ni kuendelea kuwa na mtendaji mkuu wa tume ambaye ni mtumishi wa umma, ambaye utezi wake unafanywa na rais wa nchi.

Hii ina maana kuwa mtu huyo atawajibika kwa mamlaka yake ya uteuzi. Kwamba rais siyo mtu sahihi wa kuteua mkuu wa tume ya uchaguzi, ni suala ambalo limefafanuliwa kwa muda mrefu kuonesha ubaya wake.

Ni kweli kuwa sheria mpya imeweka utaratibu wa watu wanaotakiwa kuongoza tume kuchujwa na timu maalum na baadaye majina yao kupelekwa kwa rais kwa uteuzi wa mwisho.

Sioni kama utaratibu huu una tofauti yoyote na utaratibu wa zamani kwa sababu chini ya utaratibu wa zamani, majina ya watu wanaofaa kuwa viongozi wa tume yalichujwa (ingawa yalichunjwa na vyombo tofauti na kinachopendekezwa sasa), kabla hayajatafikishwa kwa rais kwa uteuzi wa mwisho.

Tumeletewa tume huru isiyokuwa huru

Inatoka Uk. 12

Kwa hiyo kilichobadilika hapa ni chombo kinachofanya uchujaji wa watu wanaofaa kuwa viongozi wa tume katika hatua za awali kabla majina hayajapelekwa kwa rais kwa uteuzi.

Hapa maana yake ni kwamba bado rais anaendelea kuhusishwa na uteuzi wa mwisho wa kiongozi wa tume, jambo ambalo ndilo limekuwa likipigiwa kelele kwa miaka mingi.

Tungeweza kukubaliana na utaratibu huo iwapo kungekuwa na kanuni na miongozo tofauti katika utendaji wa tume, lakini hilo halipo.

Hoja hii pia inaingiliana na ule msingi wa pili wa kutofanya kazi kwa upandeleo. Hapa kwa kiasi kikubwa unazungumziwa upendeleo wa kisiasa. Rais anayemteua mkuu wa tume pia ni mwenyekiti wa chama cha siasa kilichopo madarakani.

Anapokuwa na uamuzi wa mwisho kuhusu mtu atakayesimamia uchaguzi ambao utahusisha pia chama chake, lazima kutakuwa na mashaka kuhusu uhuru wa mtu huyo kufanya kazi bila kupendelea chama cha mtu aliyemteua.

Suala la uwazi halihitaji mjadala mkubwa kwa sababu kila mmoja anafahamu umuhimu wake katika kuifanya tume ionekane inafanya kazi zake kwa uhuru, weledi na bila upendeleo.

Uwazi wa tume ili uwe na maana sana unapaswa kuwekwa kisheria na wala hatujaona jambo lolote la msingi la kuifanya tume iwe na uwazi kupitia mabadiliko ya sheria yaliyofanyika wiki iliyopita.

Msingi mwingine unaapaswa kuifanya tume ya uchaguzi ionekane kuwa huru ni kufanya kazi kwa weledi. Hapa tume inapaswa kufuata misingi fulani ya kutoa haki.

Kwanza, sheria inayounda tume inapaswa kuipa tume uhuru wake kamili wa kujitungia kanuni kwa kuwashirikisha wadau wa uchaguzi.



Masanduku ya kupigia kura

Kanuni hizo ndio zinatakiwa kutoa misingi ya weledi ambayo tume inapaswa kuifuata katika utendaji wake.

Hilo halijafanyika kupitia mabadiliko ya sheria yaliyopitishwa.

Hivyo, kuna wasiwasi mkubwa iwapo tume inayopendekezwa itafanya kazi kwa weledi unaokusudiwa.

Iwapo kiongozi wa tume atakuwa ni mtumishi wa umma, bila shaka kuwa utendaji wake utatawaliwa na miiko na misingi inayoongoza watumishi wote wa umma.

Weledi ambao utatumika katika utekelezaji wa kazi za tume utakuwa na misingi kwenye kanuni za utumishi wa umma. Sidhani kama kanuni hizo zinakidhi mahitaji ya kuifanya tume ifanye kazi kwa uhuru.

Kuhusu suala la kujitegemea, bado tunaiona kuwa tume itaendelea kutegemea bajeti yake moja kwa moja kutoka serikalini.

Kama tunataka kuifanya tume kujitegemea kifedha ni vyema ukaanzishwa mfuko maalum ambao ndio utatumika kuweka fedha zinazotumika na tume na serikali isiwe na hiyari ya kuweka fedha hizo kwenye mfuko huo ambao utakingwa kisheria.

Hii ina maana kuwa tume haitalazimika kusubiri au kuomba fedha serikalini katika utekelezaji wa majukumu yake kwa sababu shughuli zake zitakuwa zinaendeshwa na fedha kutoka katika mfuko huo maalum.

Rwanda

Mwandishi ateswa, CPJ yampigania

Na Mwandishi WETU

KAMATI ya Kimataifa ya Kulinda Waandishi wa Habari (CPJ) imesikitishwa na taarifa za kuteswa kwa Dieudonné Niyonsenga na Serikali ya Rwanda.

Jumatano ya wiki ilityopita, CPJ ilitoa mwito kwa serikali inayoongozwa na Rais Paul Kagame, kumwachilia bila masharti yeyote mwandishi huyo anayetumikia kifungo cha miaka saba jela.

Januari 10, mwaka huu, Niyonsenga alilalamika mbele ya mahakama jijini Kigali, Mji Mkuu wa Rwanda, kwamba amekuwa akiteswa, kunyanyaswa na hata kulazwa ndani ya shimo. Yupo mahakamani kwa ajili ya rufaa.

Niyonsenga ambaye pia anafahamika kwa jina la Cyuma Hassan, alifikisha mahakamani hapo akiwa na jeraha kichwani na kusema kuwa usikivu wake na maono yake yaliathiriwa kwa kipigo na mateso mengine anapoendelea kuwa kizuizini.

Mwakili wa Niyonsenga pia waliambia mahakama kwamba maofisa wa Jeshi la Magereza walimpokonya nyaraka mbalimbali za utetezi, ili kuhakikisha kuwa hapati haki yake mahakamani.

CPJ imeitaka Rwanda kumwachia mwandishi huyo bila masharti na kumruhusu kuendelea na kazi yake ya kuhabarisha umma.

Mwakilishi wa CPJ Kusini mwa Jangwa la Sahara, Muthoki Mumo amesema kinachofanywa na Rwanda ni kunyanyasa na kunyamazisha waandishi wa habari.

“Mamlaka za Rwanda zinapaswa kumwachilia Niyonsenga bila masharti, kuchunguza ushuhuda wake mchungu wa kuteswa na kuwekwa kizuizini katika mazingira ya kuzimu, na kuwawajibisha waliohusika,” aliongeza Muthoki.

Mahakama iliahirisha kesi hiyo hadi Februari 6, mwaka huu ili kumpa Niyonsenga, na mwakili wake kujiandaa kutetea hoja zao mahakamani ili haki



Dieudonné Niyonsenga

kupatikana.

Niyonsenga alichapisha maoni kwenye chaneli ya YouTube ya Ishema TV - ambayo kwa sasa haipatikani tena mtandaoni, na kukamatwa Aprili 2020, kufuatia madai kwamba alikiuka agizo la Rwanda lililowataka wananchi wote kutotoka ndani ili kujikinga na maambukizi ya Covid-19.

Ofisi ya Upelelezi ya Rwanda pia ilimfungulia mashitaka kwa madai ya kughushi leseni ya kuwa mwandishi wa habari, kujifanya mwandishi wa habari, na kuzuia utekelezaji wa kazi za vyombo vya usalama.

Niyonsenga aliachiliwa huru na mahakama ya chini Machi 2021, hata hivyo, alikamatwa tena Novemba, mwaka huohuo na kufunguliwa mashitaka yaleyale ambapo mahakama ilimkuta na hatia na kufungwa miaka saba jela.

CPJ na mashirika mengine ya kutetea haki za waandishi wa habari duniani, zimekuwa zikiandika barua kwa Serikali ya Rwanda kuhimiza kuachiwa kwa Niyonsenga, lakini hakuna majibu yanayotolewa na mamlaka ya nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Barua pepe za CPJ za Januari 29, mwaka huu kwa Wizara ya Sheria ya Rwanda na nyingine kwa Jeshi la Magereza zilizotumwa kwao hazijapata majibu hadi sasa.

Rwanda ni miongoni mwa nchi zinazotajwa kuwa na mazingira magumu kwa waandishi, ikiwamo kuteswa.



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi


Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Kitabu

Bei sh 45,000/=
DAR: Free delivery
Mikoani: delivery
sh 5,000/=



M-Pesa 0767-340-975
jina Anna



Instagram: @evarist_chahali

Twitter: @chahali

TikTok: @j.a.s.u.s.i

www.baruayachahali.com

Ujana wa Bobi wamtisha Museveni

Na Mwandishi WETU

RAIS Yoweri Museveni wa Uganda Ranaelezwa kuwa katika wakati mgumu wa kupima nguvu za mpinzani wake, Robert Kyagulanyi (Bobi Wine) baada ya kuwa na wafuasi wengi vijana “wasioeleweka msimamo wao.”

Uganda inabeba takwimu za kuwa na idadi kubwa ya vijana, ikiwa ni nchi yenye wastani wa umri wa wananchi kuwa miaka 15.9.

Vijana wenye umri wa chini ya miaka 30 ni sawa na asilimia 77 ya watu milioni 47 nchini humo, ambao ndiyo wapiga kura katika uchaguzi mkuu wa nchi hiyo. Uchaguzi Mkuu wa Uganda unatarajiwa kufanyika Januari 14, 2026.

Wachambuzi wa siasa za Uganda wanadai kuwa endapo uchaguzi ungefanyika mwaka huu, Rais Museveni asingehinda kirahisi, endapo vijana wangejitokeza kwa wingi kupiga kura.

Inaelezwa kuwa vijana wengi wana malalamiko mengi ambayo ni pamoja na ukosefu wa ajira, huku wengi wakidai kuwepo kwa upendeleo katika ajira. Wanadai kuwa fursa zimesalia kwa wachache, hasa watoto na ndugu wa wenye dhamana serikalini – hivyo, “mwokozi wao ni Bobi Wine.”

Hata hivyo, wachambuzi wanadai kuwa vijana nchini Uganda hawajaungana kuwa kambi kubwa ya uhakika wa ushindi, na ndiyo turufu anayotumia Museveni.

Katika uchaguzi uliopita wa urais wa Januari, 2021, wale walio na umri wa kati ya miaka 18 na 30 waliunda asilimia 41 ya jumla ya orodha ya wapigakura milioni 18.

Kyagulanyi, mwanamuziki aliyegeuka kuwa mwanasiasa mwenye umri wa miaka 41, ni kiongozi wa chama kikuu cha upinzani nchini Uganda, NUP – ambacho kinajulikana kwa “kuwapigania vijana” na kwamba ndicho “kinamsumbua Museveni kwa sasa.”

Mbio za Bobi Wine katika uchaguzi wa



Bobi Wine

2021 zinaangazia ukweli kwamba kupata kura za vijana nchini Uganda ni jambo gumu. Na kwamba nafasi yake ya ushindi inaenda ikiongezeka kwa kuwa na ngome ya vijana.

Wakati Bobi Wine akigombea katika uchaguzi uliopita wa urais, alikuwa na umri wa miaka 38, na alimpa wakati mgumu rais huyo wa muda mrefu wa Uganda. Museveni, 79, amekuwa rais wa Uganda tangu 1986.

Bobi Wine alipata asilimia 35 ya kura. Hii ni takriban idadi sawa ya kura ambazo zimewapata wagombea wakuu wa upinzani nchini Uganda tangu uchaguzi wa vyama vingi uanze tena mwaka 2006.

Kwa mshiriki mpya katika ulingo wa kisiasa, haya yalikuwa mafanikio ya kustaajibisha - hasa katika mwanga wa ukandamizaji wa kisiasa na ufadhili ambao unafanya uwanja kuwa mbali na haki nchini Uganda.

Kukamatwa kwa vurugu kwa Bobi Wine mnamo Novemba 2020 kulipigiwa kelele na nchi na taasisi za kimataifa, hatua ambayo iliigofya Uganda na kuamua kumuachia huru.

Kenya**Mwekezaji akana mali, ajiepusha mlipuko**

Na Mwangi MUIRURI

DERRICK Kimathi, Mfanyabiashara anayehusishwa na mlipuko wa gesi ulitokea Alhamisi iliyopita, eneo la Mradi, Embakasi, Kaunti ya Nairobi, amekana umiliki wa mali zilizoko kwenye eneo lake.

Mlipuko huo wa ghafla umesababisha vifo vya watu watatu huku wengine – wanaokadiriwa kufika 300, wakijeruhiwa. Baadhi wakiwa bado hospitali.

Anaeleza kuwa yeye ni mmiliki wa eneo na kuwa anafanya biashara nyingine, na iliyolipuka ni gesi iliyopitishwa kwenye eneo lake na dereva ambaye hamfahamu. Kwamba alipitisha gari lililobeba gesi kwa ajili ya kurekebisha.

Kimathi anadai kuwa licha ya kumiliki sehemu ambapo mlipuko huo ulitokea na kusababisha watu kupoteza maisha, mali iliyopitishwa katika eneo hilo haikuwa yake. Pia anadai mali zingine – hasa magari yaliyoegeshwa kwenye eneo lake, hazimiliki yeye.

Kupitia taarifa ya mawakili wake wawili, Wandugi Karathe na Nancy Mukabana, mwekezaji huyo amesema kwamba kinyume na dhana ambayo inaonekana kusambazwa na kupitia vyombo vya habari na pia matamshi ya baadhi ya wanasiasa, yeye pia ni mwathirika wa janga hilo sawa na wengine.

Amesema kwamba hana biashara ya gesi na iliyolipuka ilikuwa imebebwa na lori ambalo hamtambui mmiliki wake na kuwa “dereva alipitia kwangu bila idhini na hadi sasa ninashirikiana na polisi kumtia mbaroni.”

Mwekezaji huyo anasema kuwa kinyume na taswira ambayo imeundwa kwamba yeye ndiye mfanyabiashara na mwekezaji katika gesi ya mitungi inayotumika majumbani kwa kutoa kawi ya upishi, hadi wakati wa mlipuko huo utokea, alikuwa akiendesha biashara ya

*Mlipuko uliosababisha watu kupoteza maisha*

karakana ya kuunda magari.

“Ni kweli kwamba mimi nilikuwa kwa wakati mmoja nimeomba leseni ya kushiriki mauzo ya gesi ya kujaza mitungi, lakini serikali ikakataa kunipa. Niliachana na mambo hayo na hadi sasa, nimekuwa katika biashara ya uchukuzi na kuunda magari,” ameingiza Kimathi.

Amesema kwamba hata yeye anaomboleza hasara iliyotokana na mkasa huo wa moto ambao haukutarajiwa kwani ulikuwa ghafla mno.

“Aidha, hata hayo mauti yaliyozuka pamoja na majeruhi, yamenisononesha siyo haba. Pia, mimi nimeumizwa na kusambazwa kwa dhana kwamba mimi ni mhalifu wa kusababisha mauti. Ningependa nieleweke kwamba mimi ni mtiiifu wa sheria na habari zozote za kuniangazia kama mkora zinanipa huzuni,” amesema kwa masikitiko.

Kimathi aliwataka wananchi wawe na subira wakati taasisi za serikali, hasa za usalama zikiendelea na uchunguzi, badala ya kuwa na mawazo ambayo yanaweza kujenga taswira kwamba tayari yeye ni mhalifu.

Tayari serikali imeunda tume ambayo inachunguza suala hilo na kuwa itatoa taarifa ya kina baada ya kumaliza kazi yake na kuujulisha umma.

‘Mikono ya ziada’ yapaisha Afrika Kusini

Na Mwandishi WETU

JANA ilikuwa furaha kubwa kwa wananchi wa Afrika Kusini na wapenda soka, baada ya golikipa wa timu ya nchi hiyo kupangua mikwaju minne ya penati na kuiwezesha kutinga nusu fainali za michuano mikubwa ya kabumbu Afrika – Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon).

Mlinda mlango huyo, Ronwen Williams ameweka historia ya kuwa kinara golini na kustaajabisha zaidi kwa kufuata mikwaju ya wachezaji wa Cape Verde na kuipangua.

Kufuatia ushindi wa mabao 2-1, sasa Afrika Kusini itamenyana na Nigeria, kesho kutwa – Jumatano katika nusu fainali ambayo itachezwa kwenye uwanja ulioko katika Mji wa Bouake.

Timu hiyo ya taifa ya Afrika Kusini imefanikiwa kutinga nusu fainali za Afcon kwa mara ya kwanza tangu 2000, kufuatia ushujaa wa kipa wake.

Golikipa huyo ambaye hutaniwa

“kuwa na mikono ya ziada,” ameweka historia ambayo itaendelea kukumbukwa katika mchezo wake wa robo fainali ya Afcon, nchini Ivory Coast.

Mikwaju ya penati ilifanyika baada ya timu hizo mbili; Afrika Kusini na Cape Verde, zilizopambana Jumamosi kumaliza dakika 120 bila mshindi kupatikana. Mchwozo huo ulifanyika mjini Yamoussoukro.

Shuti ambalo liliharibu rekodi ya Ronwen, kuangua mikwaju yote liliwekwa kimiani na Bryan Teixeira wa Cape Verde. Mpira huo ambao golikipa alifuata, ulimponyoka.

Magoli ya Afrika Kusini yaligusa nyavu za wapinzaji wao baada ya ,ashuti ya Teboho Mokoena na Mothobi Mvala kugusa nyavu.

Golikipa Ronwen (32), ambaye ni mchezaji wa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, alizuia mpira uliopigwa na Bebe, Willy Semedo, Laros Duarte na Patrick Andrade kutinga kimiani.



Nusu fainali Afcon hiyooo...



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast wakishangilia baada ya kupata ushindi wa 2-1, dhidi ya wenzao wa Mali juzi kwenye michano ya Mataifa ya Afrika. Timu hiyo sasa inaingia nusu fainali kwa kupambana na wapinzani wao, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kesho kutwa - Jumatano. Michuano hiyo ya mwaka huu, 2024, inafanyika Ivory Coast. (Picha na Mtandao wa X wa Afcon).

GAZETI hili lilianshwa 2021, kuandaliwa na kusambaswa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

